EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA
E.L.C.T DIOCESE IN MARA REGION

TARIME PARISH
PHONE: +255784751822
+255764732622

SAMARITAN TECHNICAL SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 33, TARIME.

Email: samaritantech411@gmail.com **website: https://samaritantechnical.ac.tz.**

(NAMBA YA USAJILI S. 3884)

Tarehe:_____

Kumb. Na: ELCT/STSS/JINS/A1/2027

Jina la mwanafunzi_____
S.L. P_____
Shule aliyosoma:_____
Kata:_____
Mji/Wilaya_____
Mkoa: _____

FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA, PILI NA CHA TATU KWA WANAFUNZI WA BWENI /KUTWA - 2027.

UTANGULIZI:
Shule ya Sekondari Samaritan na Ufundi ilianzishwa mwaka 2008 na imesajiliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa namba ya usajili **S.3884.**
MAHALI ILIPO: Shule hii iko Tarime mjini katika Halmashauri ya Mji wa Tarime mtaa wa Samaritan mkabala na Goldland Hotel mita 150 na mita 5 tu kutoka kanisa la K.K.K.T.
MASOMO: Shule ni ya mchepuo wa **Sayansi** na **Sanaa**, (mkondo wa jumla) pia inatoa masomo ya **Ufundi/ mkondo wa Amali.**

MASOMO YANAYOFUNDISHWA MKONDO WA JUMLA:

1. **Basic Mathematics**
2. **English Language**
3. **Kiswahili**
4. **HistoriayaTanzania na maadili**
5. **Business study**
6. **Geography**
7. **Biology**
8. **Chemistry**
9. **Physics**
10. **History**
11. **Bible knowledge**
12. **Literature in English**
13. **Computer science(ics)**

MASOMO YA MKONDO WA AMALI:

1. **Electrical installation**
2. **Masonry & bricklaying**
3. **Graphics designs**
4. **Computer programming**
5. **Welding and metal fabrication**
6. **Carpentry and joinery**
7. **Auto electrics**
8. **Fitter mechanics**
9. **Solar power installation**
10. **Plumbing & pipe fitting**
11. **Design, sewing & cloth technology**

Shule hii ni ya mchanganyiko (wasichana na wavulana) ambao ni bweni/kutwa na inapokea maombi ya kujiunga na Muhula wa Masomo, Ambapo itaanza kupokea wanafunzi kwa muhula wa masomo mwaka **2027** kuanzia tarehe _____ ambapo wanafunzi wote wanatakiwa kuhudhuria masomo bila kukosa.

MAHITAJI MUHIMU:

Ada kwa wanafunzi wa Bweni na Kutwa:-

		BWENI	KUTWA
1.	Karo	800,000	750,000
2.	Chakula	580,000	430,000
3.	Malazi/Usafiri	250,000	150,000
4.	Uchakavu	50,000	50,000
5.	UMISETA	10,000	10,000
6.	TAALUMA	50,000	50,000
7.	Hudumaya kwanza	55,000	55,000
8.	Kitambulisho	5,000	5,000
	JUMLA	**1,800,000/=**	**1,500,000/=**

(a) **Ada iliyo ainishwa hapa chini, ni kwa wanafunzi wa Kutwa, Bweni na wageni/wanaohamia italipwa kwa awamu tatu kama ilivyokatika jedwali.**

	Januari	April	Julai	Septemba	Jumla
KUTWA	**460,000/=**	**320,000/=**	**400,000/=**	**320,000/=**	**1,500,000/=**
BWENI	**550,000/=**	**400,000/=**	**450,000/=**	**400,000/=**	**1,800,000/=**

(c). Kwa wanafunzi wanaoendelea watalipa ada kama ifuatavyo kwenye jedwali.

	Januari	April	Julai	Septemba	Jumla
BWENI	**550,000/=**	**350,000/=**	**450,000/=**	**350,000/=**	**1,750,000/=**

	Januari	April	Julai	Septemba	Jumla
KUTWA	**450,000/=**	**300,000/=**	**400,000/=**	**300,000/=**	**1,450,000/=**

Malipo yote yatafanywa kupitia akaunti za shule na Mhasibu wa shule atapokea Bank Pay – in slip na sio vinginevyo: HATUPOKEI PESA TASLIMU

AKAUNTI ZA SHULE:

1. **CRDB BRANCH. 0150042362900 (SAMARITAN TECH. SEC. SCHOOL)**
2. **NMB BRANCH. 30406600087 (SAMARITAN TECH. SEC. SCHOOL)**

(d). SARE ZA SHULE:

(i). Wavulana:

1. Suruali moja (01) Kijani nyeusi (**Dark green**) (Inapatikana **Shuleni Bure-kidato cha I**).
2. Suruali moja (01) Nyeusi (**Black**) (Inapatikana **Shuleni Bure-kidato cha I**).
3. Suruali moja (01) Bluu nyeusi (**Dark bluu) (Inapatikana Bure-kidato cha kwanza)**
4. Sweta kijani nyeusi (**Dark green) Inapatikana shuleni kwa TSh. 15,000/=**
5. Bukta na T – shirt za bluu (rangi ya Chelsea) kwa ajili ya michezo. **Inaptikana shuleni kwa Tsh. 20,000/=**
6. Tai mbili (02) moja ya kijani nyeusi na nyingine iwe ya bluu nyeusi. (Inapatikana **Shuleni Bure**).
7. **Track suit ya Bluu (Chelsea**), **T – Shirt yabluu**, na **kaptula ya Bluu** kwa ajili ya michezo na mazoezi. **Inapitikana shuleni kwa TSH.25,000/=**
8. **T-SHIRT** mbili za damu ya mzee zenye colar (**Zinapatikana Shuleni Bure-wote**)
9. Shati mbili (02) Nyeupe za mikonomifupi. (**Nunua**)
10. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba jozi mbili. (**Nunua**)
11. Soksi nyeupe jozi mbili. (**Nunua**)
12. Raba jozi moja kwa ajili ya michezo. (**Nunua**)
13. Mikanda miwili rangi nyeusi kwa ajili ya kuvalia suruali. (**Nunua**)
14. Rimu mbili karatasi **(Double A) A4** kwa kidato cha kwanza (**Nunua**), kidato cha Pili hadi cha **Nne (A3) mojana (A4**) moja kwa kila aina . (**Nunua**)

(ii). **Wasichana:-**

1. Sketi moja (01) kijani nyeusi **(Dark green).** (**Inapatikana Shuleni bure-kidato cha I**).
2. Sketi moja (01) Nyeusi **(Black).** (**Inapatikana Shuleni bure-kidato cha I**).
3. Sketi moja (01) Bluu nyeusi **(Dark bluu).**(**Inapatikana Shuleni bure-kidato cha I**).
4. **T-SHIRT** mbili za damu ya mzee zenye colar (**Zinapatikana Shuleni Bure-wote**)
5. **Track suti rangi ya Bluu (Chelsea) na T – shirt ya bluu (Chelsea)** kwa ajili ya michezo na mazoezi. **Inapitikana shuleni kwa TSH.25,000/=**
6. Sweta la kijani nyeusi (**Dark green**) **Inapatikana shuleni kwa TSh. 15,000/=**
7. Tai mbili (02) moja ya kijani nyeusi na nyingine iwe ya bluu nyeusi.(**Inapatikana Shuleni bure -wote**).
8. Shati mbili (02) nyeupe mikono mifupi. (**Nunua**)
9. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba jozi mbili. (**Nunua**)
10. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili. (**Nunua**)
11. Raba jozi moja kwa ajili ya michezo na mazoezi. (**Nunua**)
12. Rimu mbili (02) karatasi (**Double A**) A4 kwa kidato cha I **kidato cha Pili, cha Tatu na cha nne Rimu A3 moja (01) na A4 moja (01). (Nunua)**

MAHITAJI MENGINEYO:

MAHITAJI YA MWANAFUNZI

1. MWANAFUNZI WA BWENI

Mwanafunzi wa bweni anatakiwa kuja na mahitaji yafuatayo:

- Mashuka mawili: **bluu kwa wavulana na pinki kwa wasichana-Yanaptikana shuleni kwa TSH.20,000/=**. Mashuka yenye rangi nyingine hayaruhusiwi.
- Chandarua, mto na foronya mbili.
- Taulo moja na ndoo ndogo.
- Kontena la chakula lenye mfuniko, kikombe na kijiko.
- Sabuni, dawa ya meno, mswaki, kiwi, mafuta ya mwili yasiyo na kemikali na vifaa vya usafi binafsi.
- **Ndala aina ya pollo** zinapatikana shulen.

2. MAHITAJI YA KILA MWANAFUNZI

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na:

- Scientific Calculator inapatikana shuleni kwa bei ya **Tsh. 30,000/=.**
- Counter Books 12.
- Mathematical Set Aina ya NATARAJ.
- Dictionary ndogo ya Kiingereza aina ya Oxford.
- Mfuko wa kubebea vitabu/daftari.
- Saa ya mkononi.
- **Ndoo ya lita 20, Fyekeo na rake 1 kwa ajili ya usafi.**
- **Mopper/Squeezer moja na mfagio mmoja softbroom.**
- Vitabu vya masomo anayosomea.

3. WANAFUNZI WA AMALI/UFUNDI

Kila mwanafunzi anayesoma **fani ya Amali/ufundi** anatakiwa kuja na **vifaa binafsi vya msingi vinavyohitajika kwa fani yake**, kwa mujibu wa maelekezo ya shule.

Fani zinazohusika ni pamoja na:

- Electrical Installation
- Welding & Metal Fabrication
- Masonry & Bricklaying
- Computer Programming
- Graphic Design
- Tailoring
- Painting
- Mechanical/Automotive
- Capentry and joinery

Orodha ya vifaa vya kila fani itatolewa na shule kulingana na fani aliyoichagua mwanafunzi.

N:B:

1. **Sare za shule zinapatikana shuleni Kwa Tsh. 85,000/=kwa wavulana na 92,000/= kwa wasichana kidato cha pili hadi cha nne**
2. **Kwa kidato cha kwanza – sare na Godoro vinapatikana shuleni bure.**
3. **Pesa ya kunyolea kwa mwaka Tshs. 10,000/= (Kila mwanafunzi bweni).**
4. **Nakala ya cheti cha kuzaliwa ni LAZIMA**
5. **Pesa kwa ajili ya ziara za kimasomo kidato cha I na cha III Ni Tsh. 100,000/= ni LAZIMA**

SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE

- **Shule ya Sekondari na Ufundi Samaritan** ni shule inayomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (K.K.K.T) Dayosisi Mkoani Mara Usharika wa Tarime Kati. Hivyo basi mwanafunzi anayejiunga na shule hii anapaswa kufuata taratibu na maadili ya shule kama ifuatavyo:-

1. Mwanafunzi anapaswa kuhudhuria **Ibada kila siku** kwa kuzingatia ratiba ya shule bila kukosa.
2. Mwanafunzi anapaswa kusoma kwa bidi na kuhakikisha kwamba anamudu wastani wa shule ambao ni ***60%. Mwanafunzi asipofikisha wastani unaohitajika atalazimika kukariri darasa au Mzazi atalazimika kumhamishia mtoto shule nyingine***. Kwa vidato vya mitihani wanafunzi watapewa mitihani ilikupima uwezo wao kabla ya kuwasajili.
3. Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vi pindi vyote darasani bila kukosa.
4. Mwanafunzi kujiamulia kufanya jambo la aina yoyote ile bila maelekezo yoyote ni kinyume na utaratibu wa shule.
5. Kama taasisi ya kidini mwanafunzi haruhusiwi kujihusisha na ulevi, kufuga kucha, nywele, ndevu, kuvaa mavazi yasiyo ya heshima, kuiga mitindo ya kihuni, kujiremba na kuhudhuria kumbi za muziki au sehemu mbalimbali za starehe.
6. Mwanafunzi wa shule ya **Sekondari na Ufundi Samaritan** anapaswa kuwa msafi muda wote na mwenye nidhamu kwa wa kubwa na wadogo.
7. **Kila mwanafunzi awapo shuleni anapaswa kutumia lugha ya Kiingereza kwa mawasiliano kwa muda wote atakaokuwa ndani ya eneo la shule.**
8. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi shuleni.

YAFUATAYO NI MAKOSA YANAYOMWONDOA MWANAFUNZI MARA MOJA SHULENI: -

1. Kuharibu/kuiba mali ya wanafunzi wenzako.
2. Lugha ya kiingereza inatumika kwa mawasiliano wakati wote katika eneo la shule.
3. Wizi wa aina yoyote ile.
4. Mwanafunzi kujihusisha na Uasherati,Ubakaji,Ushoga,Usagaji na ulevi (pombe, madawa ya kulevya kama kubeli, mirungi, bangi, cocaine).
5. Makosa ya jinai.
6. Kupigana au kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kudharau bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa.
9. Kuoa ama kuolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa mimba au kushiriki kutoa mimba.
12. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama ndani ya shule au Nje ya shule.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Utoro uliokithiri na Kuja shuleni na silaha ya aina yoyote (panga, kisu, rungu, sime, n.k
15. Kutohudhuria Ibada.
16. Kuondoka ndani ya eneo la shule bila ruhusa (mfano kuruka uzio wa shule na Kwenda nje ya eneo la shule).
17. Kuwa na simu ya mkononi shuleni, kamera au redio shuleni.
18. Udanganyifu katika mitihani yoyote hapa shuleni.

MWONGOZO WA SHULE:

- Shule kama kiwanda ni mahali pa kuandaa wataalamu watakaoliongoza Taifa katika Nyanja mbalimbali za kitaaluma kwa siku za baadaye. Maandalizi hayo yanahitaji juhudi za Pamoja baina ya mwanafunzi kutambua kuwa anakuja kupambana na kazi ngumu inayomtaka ajitoe kikamilifu na kujinyima mengi. Kwa mantiki hiyo hatutegemei mwanafunzi kujiingiza kwenye mambo yaanasa. Shule haitavumilia mwanafunzi mzembe anayetoa visingizio vya kutofanya kazi ndani na nje ya darasa. Wanafunzi wenye matatizo ya kiafya wajulikane tangu mwanzo kupitia kwa Daktari wa hospitali ya Serikali.
- Hatutakubaliana na maelezo ya mdomo kuhusu matatizo ya kiafya ya mwanafunzi, Mwanafunzi mwenye matatizo ya kiafya ni vyema apate matibabu kabla ya kujiungana Shule, kama niugonjwa usiotibika tupate taarifa kwa maandishi kutoka kwa Daktari.

MAMBO AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUFANYA:

1. Kufuata taratibu zote kama zilivyooneshwa katika ratiba ya Shule na kama zitakavyokuwa zinatolewa na Uongozi wa Shule mara kwa mara.
2. Kuwa na utii na heshima kwa wafanyakazi wote wa Shule, viongozi na raia wotekwaujumla wake.
3. Kuheshimu Bendera, wimbo wa Taifa na alama maalumu za Kitaifa.
4. Kulinda maadili yaliyo katika **KAULI – MBIU** ya Shule yaani ***Elimu kwa wote na wote kwa Mungu.***
5. Kutumia Kiingereza daima wakati wote wasaa za masomo na kwa kuwasiliana ndani ya mazingira ya Shule.
6. Kuzingatia usafi na hifadhi ya mazingira wakati wote na kilamahali anapokuwa.
7. Kushiriki kutathmini na kuheshimu kazi zote zinazotolewa na Uongozi wa Shule.
8. Kuhudhuria Shule na vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa kadiri inavyompasa.
9. Kuzingatia ahadi hii ***"nitajielimisha kwa kadri ya uwezo wangu na kutumia elimu yangu kwa faida ya wote"***

TAREHE YA KURIPOTI SHULENI.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza ***tarehe*** _____Mwanafunzi atatakiwa kufika shuleni muda uliopangwa saa 01:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni. Mara mwanafunzi afikapo atatakiwa kuripoti Ofisi ya **MKUU WA SHULE** kwa mapokezi na kusajiliwa na **MHASIBU WA SHULE** atahakikisha kuwa Mwanafunzi amekuja na mahitaji kamili ya fedha na vifaa vyote alivyoagizwa katika barua hii, vinginevyo hatapokelewa.

A. AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi, mwanafunzi tajwa hapa chini, ninathibitisha kwamba nimepewa, nimesoma na nimeelewa Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Shule. Ninaahidi kuzifuata na kuzitekeleza kwa uaminifu wakati wote nitakapokuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Samaritan na Ufundi. Ninaahidi kuheshimu Uongozi wa Shule, walimu, wafanyakazi wenzangu na wanafunzi wenzangu; kutunza mali ya shule; kuzingatia nidhamu, usafi, usalama na maadili mema; pamoja na kushiriki kikamilifu katika masomo, mafunzo ya ufundi/amali na shughuli nyingine za shule.
Jina la Mwanafunzi:

_____

Sahihi: _____Tarehe: _____

B. AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi, mzazi/mlezi wa mwanafunzi tajwa hapa chini, ninathibitisha kwamba nimepewa, nimesoma na nimeelewa Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Shule.
Ninaahidi kushirikiana na Uongozi wa Shule katika malezi, makuzi, elimu, nidhamu na maendeleo ya mwanafunzi. Aidha, ninaahidi kutoa ushirikiano unaohitajika ili kuhakikisha mwanafunzi anazingatia taratibu za shule na anapata mazingira bora ya kujifunza.
Jina la Mzazi/Mlezi: _____
Sahihi: _____Tarehe: _____

C. **AHADI YA MZAZI/MLEZI YA KULIPA ADA/KARO NA MICHANGO HALALI YA SHULE.**

Mimi, _____

S.L.P _____ Simu _____

mzazi/mlezi wa mwanafunzi ._____

anayesoma Kidato cha_____ katika Shule ya Sekondari Samaritan na Ufundi, ninathibitisha kwamba nimeelekezwa kuhusu ada/karo na gharama nyingine zinazohusika na masomo ya mwanafunzi.

Ninaahidi kulipa ada/karo kwa wakati na kwa mujibu wa maelekezo rasmi ya shule, pamoja na gharama au michango ambayo imeruhusiwa na mamlaka husika kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za elimu.

Aidha, ninaahidi kushirikiana na Uongozi wa Shule katika kusimamia malezi, nidhamu, usalama, mahudhurio na maendeleo ya mwanafunzi, pamoja na kuhakikisha mwanafunzi anapata mahitaji muhimu kwa ajili ya kujifunza na kushiriki katika shughuli za shule.

Ninaelewa kwamba kushindwa kutekeleza wajibu wa malipo kwa wakati kunaweza kuathiri huduma za mwanafunzi kwa mujibu wa taratibu na kanuni zinazotumika.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi: _____

Jina: _____

Tarehe: _____

D. UTHIBITISHO WA URAIA NA UTAMBULISHO WA MWANAFUNZI

Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni akiwa na Hati ya Kuzaliwa (Birth Certificate) au, pale inapohitajika, Hati ya Kiapo (Affidavit) iliyotolewa/kuthibitishwa na mamlaka ya kisheria inayotambulika.

Aina ya hati iliyowasilishwa:

☐ Hati ya Kuzaliwa

☐ Affidavit

☐ Nyingine: _____

E. TAARIFA BINAFSI NA HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina Kamili la Mwanafunzi

_____

2. Tarehe ya Kuzaliwa

_____

3. Mahali Alipozaliwa

Kijiji/Mtaa: _____

Kata: ._____

Tarafa: _____

Wilaya: _____

Mkoa: _____

4. Jina Kamili la Mzazi/Mlezi

_____

_

5. Ikiwa ni Mlezi, Eleza Uhusiano Wake na Mwanafunzi

_____

__

7. Namba ya Simu ya Mzazi/Mlezi

_____

__

8.

Dini_____

Dhehebu:

_____

9. Kidato Anachoingia

Kidato cha: _____

Tarehe/Mwaka wa Kujiunga: _____

F. NDUGU/WATU WA KARIBU WA KUWASILISHIWA TAARIFA MUHIMU

Tafadhali taja ndugu au watu wa karibu ambao wanaweza kuwasiliana na shule au kupokea taarifa muhimu zinazomhusu mwanafunzi endapo mzazi/mlezi mkuu hatapatikana.

i. Jina: _____
Uhusiano: _____
Simu: _____

ii. Jina: _____
Uhusiano: _____
Simu: _____

iii. Jina: _____
Uhusiano: _____
Simu: _____

ANGALIZO: Watu waliotajwa katika sehemu hii ndio watakaotambuliwa na shule kama watu wa karibu wa mwanafunzi kwa ajili ya mawasiliano muhimu na, kwa kuzingatia taratibu za shule, kutembelea mwanafunzi shuleni.

G. TAARIFA MUHIMU KUHUSU AFYA NA USALAMA WA MWANAFUNZI

Taarifa hizi zinatakiwa kutolewa kwa usahihi ili shule iweze kuchukua tahadhari na kutoa msaada unaofaa endapo mwanafunzi atahitaji huduma ya afya au msaada wa dharura.

1. Je, mwanafunzi amefanyiwa uchunguzi wa afya kabla ya kujiunga na shule?

☐ Ndiyo

☐ Hapana

Ikiwa ndiyo, tarehe ya uchunguzi: _____

2. Je, mwanafunzi ana tatizo la afya linalohitaji uangalizi maalum?

☐ Ndiyo

☐ Hapana

Ikiwa ndiyo, eleza kwa ufupi:_____
_____

3. Je, mwanafunzi ana ugonjwa wa muda mrefu au hali nyingine inayohitaji uangalizi maalum?

☐ Ndiyo

☐ Hapana

Ikiwa ndiyo, eleza:

_____
_____

4. Je, mwanafunzi ana mzio (allergy) unaojulikana?

☐ Ndiyo

☐ Hapana

Ikiwa ndiyo, eleza:

_____
_____

5. Je, mwanafunzi anatumia dawa za kudumu?

☐ Ndiyo

☐ Hapana

Ikiwa ndiyo, eleza kwa ufupi:

_____
_____

6. Taarifa nyingine muhimu kuhusu afya, usalama au mahitaji maalum ya mwanafunzi:

_____
_____

H. UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Mimi, mzazi/mlezi wa mwanafunzi tajwa katika fomu hii, ninathibitisha kwamba taarifa nilizotoa ni za kweli na sahihi kwa kadiri ya ufahamu wangu. Ninaahidi kuijulisha shule endapo kutatokea mabadiliko yoyote muhimu kuhusu taarifa za mwanafunzi, hasa zinazohusu afya, mawasiliano, makazi au mlezi.

Jina la Mzazi/Mlezi: _____

Sahihi: _____

Namba ya Simu: _____

Tarehe: _____

HITIMISHO.

"**ELIMU KWA WOTE NA WOTE KWA MUNGU"** ni kaulimbiu ya maisha bora na endelevu kwa maendeleo ya Taifa, hivyo shule inahitaji nidhamu, utii na ushirikiano toka kwa mwanafunzi, mzazi na Uongozi wa shule kwa ujumla ili kuweza kupata mafanikio bora katika makuzi yake kitaaluma na kiroho pia.

NB: Siku za kusalimia wanafunzi ni

1. ***Jumamosi ya mwisho wa mwezi wa pili***
2. ***Jumamosi ya mwisho wa mwezi wa nane na***
3. ***Jumamosi ya mwisho wa mwezi wa kumi pekee***

ZINGATIA HILO

Tafadhali fika ofisi ya walimu kwanza ili upate maelekezo, zaidi

Aidha unashauriwa kufuatilia maendeleo ya kitaaluma, kinidhamu na kiroho ya mwanao kila mwezi

"ELIMU KWA WOTE NA WOTE KWA MUNGU"

…….

ABDUL JOSEPH

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI
UFUNDI SAMARITAN
S.L.P. 33 TARIME.

EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA
E.L.C.T. DIOCESE IN MARA REGION

TARIME PARISH
PHONE: +255767951822
+255692306829
Email.Samaritan411@gmail.com

SAMARITAN SECONDARY &
TECHNICAL SCHOOL
P.O.BOX 33 – TARIME
https://samaritantechnical.ac.tz

(Reg No.S.3884)

MEDICAL EXAMINATION.

Students full Name: ……..……..Sex:…….……Form ……..……

Age …… height (In cm)……..……..
Weight……

1. Blood count…….
2. Stool Examination……...
3. Urine analysis……..
4. Syphilis and other V.D.R.L…….
5. T.B. and Leprosy Test …….
6. Eye test …….
7. Ears test …….
8. P.U.D Test …….
9. Abdominal Test …….…….
10. Plano Test …….
11. Spleen ……..
12. Asthma ……..

Additional information e.g. physical defects or impairments infection chronic of family Disease (e.g. sickle cells) inability to eat certain food etc.
……
……
……
……
……

I certify that the above student is fit/ is not fit to pursue Secondary Education.

Signature……...
Designation……..
Station……
Date ……